CHANJO ZA COVID-19: UTENGENEZAJI NA USALAMA

030321 KISWAHILI

Utengenezaji wa chanjo unaweza kuchukua miaka mingi. Hata hivyo, chanjo za kwanza za COVID-19 zilitengenezwa chini ya mwaka mmoja baada ya ugunduzi wa virusi vinavyosababisha COVID-19. Je, iliwezekanaje?

Ni muhimu kujua kwamba chanjo zilikamilisha hatua zote za majaribio na kutathmini usalama. Hakuna hatua iliyorukwa.

Chanjo za COVID-19 zinapitia hatua zote za kawaida za kuidhinisha chanjo -- utafiti, awamu tatu za majaribio, uhakiki makini na idhini nyingi.

Wakati huu, ushirikiano kati ya watafiti, serikali kuu na kampuni binafsi zilifupisha ratiba ya kawaida. Hapa kuna sababu kadhaa kwa nini mchakato ulikuwa wa haraka zaidi kwa chanjo za COVID-19:

- **Wanasayansi walikuwa na faida.** Jitihada za chanjo ya COVID-19 zimewekwa kwenye msingi wa utafiti wa mapema wa kimataifa kuhusu virusi vya korona (haswa virusi vya SARS na MERS) na maendeleo ya teknolojia ya chanjo.
- **Ufadhili ulipatikana.** Wakati mwingine kupata pesa za utafiti wa chanjo huenda ikachukua muda mrefu. Kwa chanjo ya COVID-19, serikali kuu ilitoa pesa nyingi mara moja kufadhili juhudi za chanjo.
- **Tafiti zilipishana.** Watafiti waliandikisha watu kwa awamu zote tatu za tafiti za tiba kwa wakati mmoja. Kwa sababu ya sehemu ya ufadhili wa ziada, waliweza kuendesha awamu zote tatu za utafiti kwa wakati mmoja badala ya moja baada ya nyingine.
- **Uzalishaji ulianza mapema.** Wakisaidiwa na msaada kutoka kwa serikali kuu, wazalishaji walianza kutengeneza na kufunga chanjo hizo wakati tafiti za tiba ukiendelea.
- **Mchakato haukuwa na tatizo lolote.** Chanjo mpya za COVID-19 zinaidhinishwa na Idhini ya Matumizi ya Dharura (EUA) kutoka FDA. Hii inachukua muda mfupi sana kuliko mchakato wa kawaida wa uidhinishaji. Vikundi katika ngazi ya serikali kuu haviruhusu chochote kuwacheleweshe kutathmini chanjo. Kwa mfano, FDA iliongeza wafanyakazi wengi ili kufupisha mchakato wa tathmini kutoka miezi hadi wiki.
- **Usalama kwanza.** Chanjo inaidhinishwa tu ikiwa tafiti zinaonyesha kuwa ni salama na inafanya kazi. Kadri watu wengi wanavyopewa chanjo, FDA na CDC zitakusanya taarifa kuhusu chanjo hiyo na kuendelea kutafiti jinsi zinavyofanya kazi vizuri.
- **Chanzo za utafiti zilifanya kazi.** Kwa sababu COVID-19 imeenea sana, wanasayansi wanaweza kuona haraka jinsi watu wengi waliopewa chanjo walipata COVID-19 ikilinganishwa na wangapi waliougua bila chanjo.

Tafuta "COVID-19" kwenye tovuti ya county yako ili kupata taarifa ya mahali husika.

CLACKAMAS COUNTY

COLUMBIA COUNTY OREGON

Multnomah County Health Department

WASHINGTON COUNTY OREGON

Hatua za Kuzalisha Chanjo ya COVID-19





Utafiti
Imetengenezwa kwa msingi wa tafiti za virusi vingine vya korona.

Awamu ya 1 Utafiti wa Kimatibabu
Je, chanjo ni salama?

Awamu ya 2 Utafiti wa Kimatibabu
Chanjo inafanyaje kazi?

Awamu ya 3 Utafiti wa Kimatibabu
Je, chanjo ni salama NA inafanya kazi?

Awamu za utafiti wa tiba zilipishana.

Tathmini ya FDA
FDA iliangalia data na ikatoa Idhini ya Matumizi ya Dharura (EUA) ili kuitumia chanjo.

Kikundi cha Kutathmini Usalama wa Kisayansi katika Majimbo ya Magharibi
Kimetathmini usalama na ufanisi. (Oregon, Washington, California, Nevada)

Tathmini ya Kamati ya Ushauri kuhusu Utendaji wa Chanjo (ACIP)
Imependekeza kuhusu mtu anayepaswa kupata chanjo.

Utengenezaji
Utengenezaji ulianza mapema, wakati tathmini na uidhinishaji ukifanyika.

Tuna mengi zaidi ya kujifunza

Tafiti za chanjo zinaendelea na taarifa za ulimwengu halisi zinaongezwa kila wakati kwa kile tunachokijua kutoka kwa tafiti. Takwimu hadi leo zinaonyesha chanjo ni salama sana na zina ufanisi. Bado kuna mambo ambayo tunahitaji kujifunza juu ya chanjo ya COVID-19:

- Je, kinga inayotokana na chanjo inaisha kwa muda gani?
- Je, watu waliopata chanjo bado wanaweza kueneza ugonjwa kwa wengine?
- Je, mabadiliko ya kirusi yatamaanisha chanjo mpya zinapaswa kutengenezwa katika miaka ijayo?
- Je, kuna athari nyingine zisizo za kawaida ambazo tutazijua mara baada ya mamilioni ya watu kupata chanjo? *Iwapo athari chache za dawa zitatokea (kama mnamo Aprili na Johnson & Johnson), mchakato wa utoaji taarifa na uhakiki unawaruhusu wanasayansi kuitambua kwa haraka na kuchukua hatua.*

Haya yote ni maswali mazuri ambayo yanahitaji utafiti zaidi. Lakini sio sababu za kucheleweshe kupata chanjo ambayo ni salama na inayofaa kwa watu kwa sasa.

Unaweza kuwa na maswali na shaka

Unaweza kuhisi matumaini kuhusiana na chanjo na kuwalinda marafiki na familia dhidi COVID-19. Unaweza kuhisi wasiwasi kuhusiana na kupata chanjo. Ikiwa wewe ni mtu wa rangi, unaweza kujiuliza ikiwa unaweza kuamini chanjo kutoka kwenye mfumo wa matibabu ambao umepoteza imani katika jamii yako hapo awali. Inaeleweka kuwa na wasiwasi. Pata maelezo zaidi na upate usaidizi:

- Tembelea multco.us/covid-vaccine kwa maelezo zaidi.
- Zungumza na daktari au kliniki yako. Ikiwa huna daktari, piga simu 2-1-1 au kwa Kliniki za Huduma za Msingi za Multnomah: 503-988-5558
- Piga simu au tembelea Nambari ya Usaidizi ya Jimbo la Oregon kwa msaada wa kihisia na kielekezi cha nyenzo. Si lazima uwe katika shida. 1-800-923-HELP (4357), linesforlife.org/obhsl/